

13



## UNIVERSITY EXAMINATIONS

2021/2022 ACADEMIC YEAR  
THIRD YEAR FIRST SEMESTER

MAIN EXAMINATION

FOR THE DEGREE OF BACHELOR OF EDUCATION (ARTS)  
PART TIME GROUP

COURSE CODE: KIS 401

COURSE TITLE: KISWAHILI POETRY

DATE: 24/05/2022

TIME: 9:00AM -11:00AM

---

### MAELEKEZO

Jibu maswali **matatu** pekee.

Swali la kwanza ni la **lazima**.

MUDA: Masaa Mawili (3)

KIBU observes **ZERO** tolerance to examinations cheating

**Maswali**

1. a) Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yanayofuata.

**Oa**

Oa, kwamba u muozi, uzooleo kuoa,  
Oa, mato maolezi, na mboni ukidondoa,  
Oa, maji maundazi, meupe kama 'maziwa',  
Oa, sisi ndizi ndowa, Asokuoa ni yupi?

Oa, 'maji ya kisima', yatengenwye na mvua,  
Oa, ukijitezama, kioo ukichanguwa,  
Oa, mwanamke tama, mtukufu wa sitawa,  
Oa, sisi ndizi ndowa, Asokuoa ni yupi?

Oa, ndiwe muolezi, uzooleo kuoa,  
Oa, sifumbe maozi, maninga uchiyavuwa,  
Oa, usaze uzazi, kama ulivyojaliwa,  
Oa, sisi ndizi ndowa, Asokuoa ni yupi?

Oa, watoka ngamani, uliopo ukiifuwa,  
Oa, majini ya p'wani, umeyakosa ya ziwa,  
Oa, ni hizi zamani, tulizo tukiambiwa,  
Oa, sisi ndizi ndowa, Asokuoa ni yupi?

Oa, 'maji t'imbe' imbe', mema ya mtu kuyoa,  
Oa, maozi sifumbe, nawe utafurahiwa,  
Oa, uole wapambe, wako uliopambiwa,  
Oa, sisi ndizi ndowa, Asokuoa ni yupi?

Oa, unoweza nami, unowezapo t'akoya,  
T'akoya saya maumi, maumi ya kuumia,  
Umia nyama za nyemi, nyemi za kunyemenyea,  
Nyea kutombonekea, ambonea ni yupi?

- a) Eleza maudhui yoyote matatu katika shairi hili. (alama 6)
- b) Jadili sitiari tatu zinazojitokeza katika shairi hili. (alama 6)
- c) Liweke shairi hili katika bahari zozote tatu kwa kutolea sababu. (alama 6)
- d) Eleza maana yoyote mbili ya neno 'Oa' katika muktadha wa shairi hili. (alama 2)

b) Bainicha maandalizi yoyote matano ya kisaikolojia ambayo mwalimu anaweza kuyafanya ili kuufanya ushari kuwa mwepesi kwa wanafunzi. (alama 10)

2. Changanua namna diwani ya *Dhifa* inavyosawiri maudhui ya jamii ya sasa. (alama 20)

3. Jadili namna zozote tano ambazo mtunzi wa *Al-Inkishafi* alivyosawiri dunia katika utunzi wake. (alama 20)

4. Kwa kuzingatia hoja zozote tano, jadili sababu zilizopelekea mgogoro kutokea katika ushairi wa Kiswahili. (alama 20)

5. Kwa kutoa mifano katika diwani ya *Doa* au *Msimu wa Tisa*, pambanua dhamira ya mwandishi kwa kurejelea hoja zozote tano. (alama 20)